

Utunzaji wa afya

Sharti mbuzi wapewe dawa za minyoo mara kwa mara na wanyonyiziwe dawa ili kuwaua wadudu kama vile kupe, viroboto na chawa.



Healthy goats



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Korir, B.K.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI Kiboko, S.L.P. 12, Makindu 90138

Simu: (045) 223667/8

Nukulishi: (045) 622314

Baruapepe: kari.kiboko@yahoo.co.ke

Vijitabu ya KARI ya taarifa, nambari / 20 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Ufugaji mbuzi katika sehemu kame za Kenya



Utangulizi

Ukuzaaji wa mbuzi katika sehemu kame za Kenya huhadhiriwa na:

- Maradhi na magonjwa yaletwayo na wadudu
- Aina za hali ya chini na maakuli yasiyofaa
- Lishe za hali ya chini
- Kuingiliwa na wadudu.

Makaazi bora, ushalizaji unaofaa na lishe mwafaka ni mbaadhi ya njia zinazoweza kusuluuhisha hali hii na kupunguza vifo nya mbuzi watoto.


Maakazi

Vyumba vinafaa kuwa na hewa na, mwangaza tosha, visiwe na baridi. Vyumba mwafaka hukinga wanambuzi kutokana na hali kali za anga ambazo huweza kuwaletea homa ya mapafu.

Makaazi pia husaidia:

- Utunzaji wa kibinagsi
- Kuzuia wanyama pori na wizi
- Uokotaji wa mbolea.

Usafishaji wa kila mara hupunguza kuwepo na kupe na wadudu wengine na mbolea hutumika kuimarisha mimea.



Chumba cha mbuzi chenyehewa halisi

Uzalishaji

Aina ya uzalishaji au ukoo wa mbuzi atakayezalishwa na utunzaji wake ni vipengele muhimu katika ukuzaaji wa mbuzi. Aina ambazo hupatikana kwa wingi katika sehemu kame ni *Gala (Somali)* na *Small East African*. (Mbuzi mdogo wa Afrika mashariki).

Mbuzi wanahitaji kupewa dume ili msimu wa kuzaa uwe sambamba na nyakati ambapo kuna vyakula nya kutosha nya mbuzi ili wanambuzi wengi wazaliwe na pia kuongeza uwezekano wa kupata mapacha.

Nyakati za kunyonyesha wanambuzi pia zinafaa kuwa wakati ambapo kuna malisho ya kutosha ndio wanambuzi wapate maziwa ya kunyonya ili wakue haraka.

Wanambuzi ambaa hukua haraka hubalehe mapema na pia hustahimili changamoto za maradhi.



Mwanambuzi akinyonya

Kuzalishana baina ya boma kunaweza kuelpukwa kwa kuondoa mbuzi wa kiume kwa boma.

Pia, kijifuko kinachovishwa mbuzi wa kiume ni njia

nyingine mwafaka ya kuzuia mimba zisizohitajika.

Mbuzi-dume wanahitaji kubandilishwa punde mbuzi wa kike wanapofikia umri wa kuzaa.



Mbuzi-dume amevalishwa kijifuko

Malisho

Ubora na kiasi cha malisho ni changamoto kubwa hasa wakati wa kiangazi.

Uhifadhi wa lishe husaidia sana wakati kuna upungufu na unaweza kufanywa kwa kupanda mimea yenye matumizi kadhaa kama vile mtama, mbaazi na njahi (*dolichos*).

Mbinu zingine za kuhakikisha kuwepo kwa lishe ni kama vile:

- kuokota mbegu za *acacia* na kuzihifadhi zitumiwe nyakati za upungufu wa malisho.
- Kutenga kando sehemu za malisho na kupanda maakuli ya hali bora.
- Kuhakikisha kuwepo maji wakati wote na hasa mbuzi wanapohara.